Toleo la Novemba 2024

# Fama

**JARIDA LA KILIMO, UFUGAJI NA UJASIRIAMALI**

# NFRA yaja na hatifungani



## BODI YA WAHARIRI

**JESSE KWAYU**
+255 767 328 446
AFISA MTENDAJI MKUU NA MHARIRI MTENDAJI MKUU

**ABSALOM KIBANDA**
+255 754 001 010
MHARIRI MTENDAJI

**NEVILLE MEENA**
+255 753 555 556
MHARIRI MKUU

**DENIS MSACKY**
+255 747 444 401
MHARIRI MSHIRIKI

**MATANGAZO**
+255 767 328 446
+255 754 001 010
+255 753 555 556

**HUTOLEWA NA KAMPUNI YA BRAIN INC. LTD**
KINONDONI 'B'
S.L.P 3457,
DAR ES SALAAM,
TANZANIA
TEL: +255 787 32 9600
EMAIL:
FAMA@THEMEDIABRAINS.COM
HUCHAPWA NA TANZANIA PRINTERS

## YALIYOMO



04 MAFURIKO KUGEUZWA FURSA YA UMWAGILIAJI



07 NEEMA MIKONONI MWA WANAWAKE, VIJANA



10 MWANZO AU MWISHO WA MAPAMBANO?



14 USICHUKULIE MBEGU YA MIWA POA, INAHITAJI MIAKA 15 KUMFIKIA MKULIMA



17 MLIMA WA KUFIKIA HIFADHI TANI MILIONI MOJA

# TAHARIRI

## Mageuzi ya kilimo yatawezekana tu kwa umwagiliaji

URUSI ilipoivamia Ukraine Februari 24 mwaka 2022 ghafla dunia nzima ilipata madhara makubwa ya upungufu wa nafaka ya ngano pamoja na bidhaa zake. Upungufu huo ulitokana na shehena ya ngano ambayo hulimwa kwa wingi Ukraine kushindwa kusafirishwa. Kwa maana hiyo dunia nzima ilipata upungufu wa bidhaa za jamii ya ngano kwa sababu tu matatizo yalitokea Ukraine.

Ukiitazama Ukraine yenye ukubwa wa kilometa za mraba 603,628 ikiwa na ardhi ifaayo kwa kilimo yenye ukubwa wa hekta milioni 41.3, ni ndogo kuliko eneo lote la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenye ukubwa wa kilometa za mraba 945,087 ikiwa na ardhi ifaayo kwa kilimo yenye ukubwa wa hekta 44. Kwa ulinganifu huu unaweza kujihoji ni kwa nini Tanzania siyo mzalishaji mkubwa wa zao lolote duniani kiasi kwamba iwe ndiyo tegemeo kuu?

Hali ya Tanzania kutokuwa na nguvu kubwa sana katika uzalishaji wa mazao ili iwe tegemeao kubwa la usalama wa chakula la dunia, inaweza kufungamanishwa na mfumo wetu wa kilimo cha kutegemea mvua. Mazao mengi yanayolimwa nchini hapa kwa kiwango kikubwa yanategemea mvua. Kama mvua hazikunyesha, basi huo unakuwa ni mwaka wa hasara siyo kwa wakulima tu, bali pia kwa usalama wa chakula nchini.

Ni katika kutambua umuhimu wa kujiweka kwenye nafasi ya kuwa mzalishaji mkubwa wa mazao mbalimbali ya kilimo, kama mahindi, maharage, ufuta, alizeti, michikichi, pamba, kahawa na mazao mengine ya mbogamboga, serikali imeamua kuingia katika kazi kubwa ya kuleta mageuzi katika kilimo kwa kusukuma mbele ajenda ya kilimo cha umwagiliaji.

Miongoni ni mwa juhudi hizi ambazo tunasema zinastahili kuungwa mkono na kutengewa fedha za kutosha, ni mkakati wa kufufua skimu zote za umwagiliaji nchini, pia kujenga mpya ili kuongeza uwezo wa taifa kuendesha kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha umwagiliaji kinatoa fursa kwa wakulima kufanya kazi ya uzalishaji mashambani mwaka mzima, tofauti na kilimo cha kutegemea mvua.

Katika kufanikisha mkakati huo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC) imeingia makubaliano na Shirika la Reli Tanzania (TRC) ili kujenga mabwawa sita kwenye ukanda wa Reli ya Kati maeneo ambayo yamekuwa korofi kwa mafuriko. Maeneo ambayo mabwawa haya yanakwenda kujengwa kuanzia mwaka wa fedha wa 2024/25 ni pamoja na Dabalo, Buigiri, Hombolo, Kimangae, Kidete na Ikowa. Maeneo haya yanapatikana katika mikoa ya Morogoro na Dodoma. Kujengwa kwa mabwawa haya kutaongeza shughuli za kilimo cha uhakika na hivyo kuongeza thamani ya adhi ifaayo kwa kilimo nchini.

Mbali na mabwawa haya, pia serikali inatekeleza miradi mingine ya umwagiliaji katika maeneo tofauti nchini ambako jumla ya miradi 780 yenye thamani ya Sh. bilioni 366.5 inatekelezwa. Miradi hii ilianza kutekelezwa kuanzia mwaka wa fedha wa 2022/23 na kazi inaendelea.

Ingawa serikali imekusudia kuongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji hadi kufikia hekta milioni 1.2 ifikapo mwaka 2025, matarajio halisi ni kwamba hekta 983,466.06 sawa na asilimia 81.95 ya lengo zitapatikana ifikapo mwaka 2025. Ni matamanio ya umma wa Watanzania kwamba kwa neema ya ardhi ifaayo kwa kilimo ambayo nchi hii imejaliwa sasa tutaanza kujiweka kwenye nafasi ya kuwa nchi tegemewa kwa uzalishaji wa chakula duniani. Hali hii siyo tu itatujengea heshima, bali itasaidia kujenga uchumi imara wa nchi na kwa mwananchi mmoja mmoja.

Kwa miaka na miaka nchi yetu imekuwa inasumbuliwa na mafuriko ya mara kwa mara kutokana na kupata mvua nyingi, hata hivyo badala ya kutumia mvua hizo kujenga akiba kubwa ya kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, tumekuwa tulilalamika huku tukipoteza rasilimali hiyo adhimu kwa kujaza bahari.

Sisi tunaamini Ukraine imejiweka kwenye nafasi hiyo ya kuwa tegemeo kubwa la nafaka ya ngano duniani kwa sababu wamewekeza kwenye kilimo, wamejenga miundombinu ya kusaidia kilimo kuwa shughuli yenye tija kubwa. Ni kwa kufuata nyayo kama hizo tu ndipo nasi kama taifa tunaweza kunufaika na adhi kubwa ifaayo kwa kilimo ambayo Mola ametukirimu.



# Mafuriko kugeuzwa fursa ya umwagiliaji

**Moja ya miundombinu ya umwagiliaji inayosimamiwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC). Picha kwa hisani ya NIRC**

**"SERIKALI INAJENGA MABWAWA MAKUBWA MIKOA YA DODOMA NA SHINYANGA KATIKA MAENEO YA MEMBE, MSAGALI, KASOLI, KATUNGURU, MKOMAZI NA EYASI ILI KUHAKIKISHA WAKULIMA WANAPATA MAJI YA KUTOSHA KWA KILIMO CHA UMWAGILIAJI HATA KWENYE MSIMU WA KIANGAZI, TUNATAKA MIRADI YA UMWAGILIAJI IKAMILIKE KWA UJUMLA WAKE, KUANZIA KWENYE CHANZO CHA MAJI, VIBANIO HADI MASHAMBANI," ANASEMA TENGENEZA.**

**NA NEVILLE MEENA, FAMA**

UJENZI wa visima na mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji umeshika kasi nchini, huku kukiwa na jitihada za kuyageuza maafa ambayo husababishwa na mafuriko, kuwa fursa kwa wakulima. Miundobinu hii inayojengwa sasa ni kama mwelekeo mpya katika utafutaji wa vyanzo vya upatikanaji wa maji kwa ajili ya kufanikisha kilimo hicho.

Katika mwaka huu wa fedha (2024/2025) Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC) kwa kushirikiana na Shirika la Reli Tanzania (TRC) imepanga kuanza mchakato wa ujenzi wa mabwawa sita yatakayotumika kuzuia mafuriko katika reli ya kati na wakati huohuo maji yake kutumika kwa shughuli za kilimo cha umwagiliaji.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, anasema NIRC kwa kushirikiana na TRC wataanza kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya mabwawa hayo sita ambayo anayataja kuwa ni Dabalo, Buigiri, Hombolo, Kimagae, Kidete na Ikowa. Maeneo yanayotajwa yanapatikana katika mikoa ya Morogoro na Dodoma.

Kwa mujibu wa Wizara ya Kilimo, miudombinu hiyo (mabwawa na visima) ni sehemu ya miradi 780 ya umwagiliaji yenye thamani ya Sh. bilioni 361.5 iliyoanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 na utekelezaji huo kuendelezwa katika mwaka 2023/2024.

Kwa mujibu wa Mhandisi Mwinchuma Tengeneza, ambaye ni Msimamizi wa Ujenzi na Ukarabati wa Miondombinu ya Umwagiliaji, serikali imewekeza fedha nyingi katika ujenzi wa miradi ya

umwagiliaji na kwamba uwekezaji huo, unagusa miradi inayotekelezwa katika mikoa yote 25 nchini.

Tengeneza anasema utekelezaji wa miradi hiyo unaanzia kwenye chanzo cha maji hadi mashambani. Katika mpango huo serikali imejikita kujenga mabwawa makubwa ambayo yatatumika kuhifadhi maji kwa ajili ya matumizi ya kilimo wakati wa kiangazi, ili wakulima waweze kulima misimu miwili au mitatu kwa mwaka.

"Serikali inajenga mabwawa makubwa mikoa ya Dodoma na Shinyanga katika maeneo ya Membe, Msagali, Kasoli, Katunguru, Mkomazi na Eyasi ili kuhakikisha wakulima wanapata maji ya kutosha kwa kilimo cha umwagiliaji hata kwenye msimu wa kiangazi, tunataka miradi ya umwagiliaji ikamilike kwa ujumla wake, kuanzia kwenye chanzo cha maji, vibanio hadi mashambani," anasema Tengeneza.

Visima na mabwawa ni nyongeza kwenye njia nyingine za umwagiliaji ambazo zinategemea vyanzo asili vya upatikanaji wa maji, hasa vile vinavyowezesha rasilimali hiyo kupatikana kwa njia ya mserereko; kwamba vyanzo vingi vya maji huwa milimali au kwenye sehemu zenye miinuko na huelekezwa mabondeni au maeneo ya tambarare ambako ndiko kuna mashamba yanayohitaji kumwagiliwa.

Hata hivyo, upatikanaji wa maji kutokana na vyanzo vya asili umekuwa ukikabiliwa na changamoto kadhaa zikiwamo za ukame wa muda mrefu na kusababisha miundombinu ya umwagiliaji kukosa maji kama ilivyotokea wakati wa msimu wa



**Moja ya miundombinu ya umwagiliaji inayosimamiwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC). Picha kwa hisani ya NIRC**

kilimo wa mwaka 2022/2023.

Kutokana na ukame wa kipindi hicho, Novemba 2022 baadhi ya skimu za umwagiliaji wilayani Gairo mkoani Morogoro zilishindwa kufanya kazi kutokana na ukame uliosababisha kukosekana kwa maji, hivyo kuathiri kilimo cha mbogamboga na matunda.

Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya hiyo wakati huo, Jabir Makame, alinukuliwa na vyombo vya habari akieleza kukakuka na kutoweka kwa baadhi vyanzo vya maji wilayani humo, zikiwamo chemchemi za asili.

Katika mazingira hayo ni dhahiri kwamba mbadiliko ya tabia nchi yamekuwa na athari

kubwa hata kwenye vyanzo vya maji vya asili, hivyo kuvifanya kutegemea mvua kama

ilivyo kwa shughuli za kilimo katika maeneo mengi nchini.

**HALI YA UMWAGILIAJI HADI MEI 2024**

| | |
|---|---|
| Malengo ya umwagiliaji hadi 2025 | Hekta 1,200,000 |
| Eneo lilokuwa likimagiliwa hadi msimu wa 2023/2024 | Hekta 727,280.6. |
| Ujenzi na ukarabati msimu wa 2022/2023 - 2023/2024 | Hekta 256,185.46 |
| Eneo zima tarajiwa la umwagiliaji | Hekta 983,466.06 |
| Chanzo: Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo mwaka 2024/2025 | |

Waziri wa Kilimo Hussein Bashe akiwasilisha bajeti ya Wizara hiyo bungeni alisema ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji unaoendelea, utawezesha eneo linalomwagiliwa kufikia hekta 983,466.06 ambazo ni sawa na asilimia 81.95 ya lengo la hekta 1,200,000 ifikapo 2025 kama ilivyoelekezwa kwenye Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025.

Kwa mujibu wa Bashe Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa mwaka 2024/2025 inaendeleza utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji 780 ukiwa ni mwendelezo wa miradi 133 iliyoanzwa kutekelezwa mwaka 2022/23 na miradi 647 iliyoanza kutekelezwa mwaka 2023/2024.

Miradi hiyo inajumuisha ujenzi wa visima ukiwa ni utekelezaji wa mpango wa kuchimba visima kwa wakulima wadogo kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika eneo lenye ukubwa wa ekari 2.5, uliozinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwenye Maonesho ya Kimataifa na Sikukuu za Wakulima – Nanenane ya mwaka 2023 yaliyofanyika Viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya.

Kadhalika Rais Samia kwenye maonesho ya mwaka 2024 yaliyofanyika Viwanja vya Nzuguni, Dodoma alizungumzia kilimo cha umwagiliaji akisema upo umuhimu kwa wakulima kufundishwa mbinu

za unyunyuziaji (umwagiliaji wa matone - drip irrigation) badala ya umwagiliaji, ikiwa ni hatua ya kuzingatia matumizi bora ya maji.

"Naiagiza Wizara ya Kilimo kutoa elimu kwa wananchi juu ya utunzaji na uendelezaji wa vyanzo vya maji, tuanze unyunyuziaji wa mazao badala ya umwagiliaji ili kutunza na kuhifadhi maji yanayopotea," alisema Rais.

**Ujenzi wa Visima**

Kwa mujibu wa NIRC, ujenzi wa visima unatekelezwa chini ya mradi wa P4R (Food System Resilience Program), unaofadhiliwa na Benki ya Dunia na wafadhili wengine kwa gharama ya dola za Marekani milioni 70 (takribani Sh. bilioni 190.7).

Mhandisi Mwandamizi wa NIRC, Naomi Mcharo anasema mradi huo unatekeleza mambo makubwa matatu; kuwezesha upatikanaji wa maji kwa wakulima wadogo, ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji na kuimarisha usimamizi na matunzo ya miundombinu.

Mcharo anasema chini ya mpango huo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kuchimba visima 1,000 katika mwaka wa fedha 2023/2024. Kazi ambayo utekelezaji wake utahusisha kampuni zinazomilikiwa na wazawa ambao watalazimika kuingia kwenye ushindani kupitia zabuni zitakazotangazwa.

Anasema katika kufanikisha ujenzi wa visima hivyo, NIRC imepanga kununua mitambo itakayotumika kuchimba visima hivyo ikiwatumia wahandisi wake wapya zaidi ya 100 walioajiriwa mwaka jana. Ajira hizo ni hatua ya Tume hiyo kujenga uwezo wa kutekeleza baadhi ya shughuli zake badala ya kutegemea wataalmu wa nje ya taasisi hiyo.

Katika kufanikisha mradi huo, Mcharo anasema Halmashauri za Wilaya nchini zimeshirikishwa katika utekelezaji, kwa kuainisha maeneo 150 yanayofaa kwa ajili ya kuchimba visima hivyo.

Hata hivyo, anasema kwa kuanzia katika mwaka wa fedha 2024/25 visima vitakavyochimbwa nchi nzima kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji ni 1,000 na kila halmashauri itapata visima vitano.



Skimu ya umwagiliaji Madibira iliyoko Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya.



"Visima hivi vitachimbwa kwa ushirikiano na Halmashauri za Wilaya, maeneo yamechaguliwa na kuhakikiwa kwa ushirikiano na Wakuu wa Wilaya kuepusha migogoro kwa sababu maeneo hayo yanatumiwa na jamii," anasema Mhandisi Mcharo.

Waziri wa Kilimo Bashe aliliambia Bunge kuwa Tume ya Umwagliaji imepanga kununua mitambo ya kuchimba visima na katika mwaka 2024/2025 itaanza na ununuzi wa mitambo 30.

"Mitambo hiyo itatumika katika uchimbaji wa visima katika Halmashauri mbalimbali nchini," alisema Bashe.

**Ujenzi wa mabwawa**

Taarifa za Wizara ya Kilimo zinaonesha kuwa kati ya miradi ya umwagiliaji 133 iliyoanza kutekelezwa mwaka 2022/2023, imo 14 ya ujenzi wa mabwawa ambayo yakikamilika yatakuwa na uwezo wa kuhifadhi mita za ujazo 131,535,000.

Kadhalika taarifa zaidi zinasema kati ya miradi 647 iliyopangwa kutekelezwa na Tume ya Umwagiliaji katika mwaka wa fedha 2023/2024, kulikuwa na kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabwawa mapya 100 pamoja na kuanza ujenzi wa mabwawa hayo yenye takribani mita za ujazo 936,535,700.

Bashe anasema ujenzi wa mabwawa hayo 100 utaendelea katika mwaka wa fedha 2024/25, lengo likiwa ni kuwezesha uvunaji wa maji kwa kwa ajili ya umwagiliaji na kwamba upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa bonde la mto Ngono na Bugwema mkoani Kagera umekamilika na sasa hatua za kumtafuta mkandarasi kwa ajili ya ujenzi zinaendelea.

"Tume ya Umwagiliaji itakamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa bonde la Mto Rufiji. Mwaka 2024/2025 itaanza ujenzi wa mabwawa mawili Mbakiamtuli na Ngorongo, ujenzi ambao unatarajiwa kutakamilika ndani ya miaka mitatu," anasema Bashe na kuongeza: "Tume pia itanunua mitambo mitatu (3) kwa ajili ya uchimbaji wa mabwawa ya umwagiliaji."

# MBEYA FOOD PARK:

## Neema mikononi mwa Wanawake, Vijana



Baadhi ya wajasiriamali wakifungasha vikolezo vya mboga vilivyosindikwa na moja ya mashine zilizopo ndani ya Mbeya Food Park tayari kwa kupelekwa sokoni. Picha na Neville Meena

**NA MWANDISHI WETU, MBEYA**

MRADI wa Kilimo bora cha Mbogamboga na Matunda kwa Wanawake na Vijana (KIBOWAVI) umehitimisha safari yake ya miaka minne katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya, Katavi na Songwe), huku ukiacha alama na historia ya kukumbukwa kwa wanufaika wake katika mikao hiyo.

Mradi wa KIBOWAVI unatekelezwa katika Halmashauri 11 katika mikoa hiyo na umewafikia zaidi ya watu 80,000 (wakulima na wasindikaji 21,334) na  (wanawake 12,801 vijana 8,533). Hawa wamenufaika na mafunzo ya mbinu bora za kilimo, elimu ya lishe, elimu ya biashara na usimamizi wa fedha, elimu ya jinsi na jinsia, mafunzo ya kuzuia upotevu wakati na baada ya mavuno na kuongeza thamani mazao. Pia wamejenga vituo 11 vya mafunzo kwa wakulima.

Mradi huo ulianza Februari 2020 na kuhitimishwa Februari 2024, ukifadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) chini ya Programu ya AGRI-CONNECT na kutekelezwa na shirika la HELVETAS pamoja na washirika wake; TAFOPA, CODERT na ADP Mbozi.

TAFOPA ni kifupi cha Tanzania Food Processing Association (taasisi isiyo ya kiserikali inayojihusisha na usindikaji wa vyakula mbalimbali nchini), wakati CODERT ni kifupi cha Community Development and Relief Trust (Shirika la Misaada na Maendeleo ya Jamii linalofanya kazi zake hapa nchini na ADP ni kifupi cha Action for Development Program ambalo shirika lisilo la kiserikali linaloendesha shughuli zake Tanzania bara, likifanya kazi zake mkoani Mbozi mkoani Songwe.

Lengo kuu la mradi huo lilikuwa ni kuchangia ukuaji wa uchumi jumuishi, kuendeleza sekta binafsi na kuzalisha ajira katika mnyororo wa thamani wa mazao ya mbogamboga na matunda. Pia kuimarisha upatikanaji wa chakula na lishe katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania.

Miongoni mwa alama kuu ambazo zimeachwa na mradi huo ni kiwanda cha usindikaji wa mboga, matunda na viungo (Mbeya Food Park) kilichopo uwanja wa ndege wa zamani wa Mbeya, Kata ya Iyela. Baada ya ujenzi wake kukamilika kilikabidhiwa kwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya kwa ajili ya usimamizi na uendeshaji.

Kiwanda hicho kilichoanza kujengwa mwaka 2021 na kukamilika mwaka 2023 kinabeba taswira nzima ya mradi wa KIBOWAWI. Jengo lake linajumuisha sehemu ya kupokea na kusafisha malighafi, sehemu ya uzalishaji, maabara, sehemu ya kuhifadhia



Baadhi ya wajasiriamali ndani ya Mbeya Food Park wakipokea tangawizi inayotoka katika moja ya mashine za usindikaji katika kiwanda hicho.

**KIWANDA KINAJUMUISHA MAJENGO NA MASHINE ZAKE ZA USINDIKIKAJI AMBAVYO VIMEGHARIMU SH.1,719,582,174 (EURO 663,071). KATI YA HIZO JENGO NI SH. BILIONI 1.33, MASHINE MBALIMBALI SH. MILIONI 309 PAMOJA NA VIKAUSHIO, KISIMA NA VIFAA VINGINE AMBAVYO GHARAMA ZAKE NI SH. MILIONI 77.55.**

bidhaa na duka la kuuzia bidhaa.

Kiwanda hicho kilizinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango Julai 3, 2023, kama sehemu ya shughuli za utangulizi, kabla ya maonyesho ya Kitaifa ya Kilimo (Nanenane) yam waka 2023.

Kiwanda kinajumuisha majengo na mashine zake za usindikikaji ambavyo vimegharimu Sh.1,719,582,174 (Euro 663,071). Kati ya hizo jengo ni Sh. bilioni 1.33, mashine mbalimbali Sh. milioni 309 pamoja na vikaushio, kisima na vifaa vingine ambavyo gharama zake ni Sh. milioni 77.55.

Fedha hizo ni sehemu ya bajeti ya mradi mzima ambayo ilikuwa jumla ya Euro 5,000,000, fedha ambazo zilichangwa na Umoja wa Ulaya – EU kwa kiasi cha asilimia 90, wakati ushirikiano (consortium) ulioongozwa na HELVETAS na wadau wake walitoa asilimia 10. Washirika wa mradi huo walioogozwa na HELVETAS ni TAFOPA, CODERT na ADP MBOZI.

**Malengo ya ujenzi wa kiwanda**

Mkurugenzi wa Programu ya HELVETAS – KIBOWAVI, Daniel Kalimbiya, anasema kiwanda hicho kilijengwa kwa lengo la kutatua changamoto zinazowakabili wakulima na wasindikaji wengi wadogo na kati.

Changamoto hizo ni pamoja na upotevu wa mazao baada ya mavuno na ukosefu au upungufu wa maeneo safi na salama ya kusindika bidhaa. Ukosefu huo uliwafanya wazalishaji wengi kusindikia bidhaa nyumbani, hivyo kukosa nembo za ubora na kusababisha kutokukidhi vigezo vya masoko mbalimbali yakiwamo ya ndani na nje ya nchi.

Anasema HELVETAS na wadau wake walijenga kiwanda hicho na miundombnu katika maeneo mengine ya mradi kwa ajili ya kuongeza thamani mazao ya bustani (mbogamboga, matunda na viungo) ili kuwasaidia wakulima na wasindikaji wadogo na kati kutatua changamoto hizo.

Kwa mujibu wa Kalimbiya mradi huo umepata mafanikio ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa kikundi cha wasindikaji Mkoa wa Mbeya chenye wanachama zaidi ya 200. Vijana 20 waliajiriwa kiwandani wakiwa na majukumu ya kusimamia shughuli za kila siku (wataalamu, watu wa usafi na walinzi) na ajira 206 za muda zimetengezwa kwa ajili ya kazi za kuandaa malighafi, kupaki na kuuza bidhaa zilizosindikwa.

"Jumla ya wasindikaji wa mazao ya bustani 14 wamepanga katika kiwanda hiki, ambao pia wamekuwa wanunuzi wa malighafi kutoka kwa wakulima na katika muda mfupi kama miezi sita tani 15,192.41 za mazao ya bustani zimechakatwa na kuongezewa thamani," anasema Kalimbiya.

Mmoja wa wanufaika wa Mradi, Fatuma Mbaga (27) anasema: "Kabla ya mradi huu hali yangu katika usindikaji wa viungo haikuwa nzuri kukidhi viwango vya soko, lakini baada ya msaada wa mafunzo na miundombinu ya usindikaji, nimemudu kusindika viungo vya ubora vinavyokidhi viwango vya soko la kitaifa (TBS) na kimataifa. Hivyo, nimeweza kupata soko




**Jengo la Mbeya Food Park ambamo zimewekwa mashine za kusindika mazao mbalimbali. Chini (kushoto) ni mashine ya kusukuma maji ya umwagiliaji inayotumia umemejua (solar) na kulia ni eneo la shamba la mfano lililopo katika eneo hilo.**

mpaka nchini Marekani na kuajiri wafanyakazi wengine saba (7) wa kudumu."

Kiwanda hicho kinasimamiwa na Bodi ya Usimamizi ambayo inaundwa na wajumbe wanaowakilisha Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wasindikaji/wanufaika, HELVETAS, TAFOPA, SIDO, CODERT, ADP Mbozi, baadhi ya benki na Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya.

Anasema kampuni ya SUMA JKT imeajiriwa kwa ajili ya ulinzi na usalama wa kiwanda na mali zake.

Kiwanda kimekuwa kikipokea wanafunzi wa vyuo vikuu kwa ajili ya mafunzo ya vitendo na ufanya tafiti. Mafanikio mengine ni baadhi ya bidhaa kupata nembo ya ubora kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), huku sampuli nyingine zikichuliwa na mamlaka hiyo kwa ajili ya kuchunguzwa kabla ya kupewa nembo za ubora.

"Jengo hili pia lina ofisi za wafanyakazi, vyumba vya kubadalishia nguo na kupangisha wasindikaji, sehemu ya mashine na ofisi za watumishi. Pia lina sehemu za kuhifadhia bidhaa na duka la kuuzia bidhaa (supermarket)," anaseme Kalimbiya na kuongeza kuwa kiwanda hicho pia kimeunganishwa na umeme wa Tanesco, nishati ya umeme wa jua na mfumo wa kamera ndani na nje ili kuimarisha ulinzi.

Miundombinu mingine iliyojengwa kupitia HELVETAS - KIBOWAVI kupitia mradi huo ni pamoja na maghala mawili ya kuhifadhi vitunguu na iliki wilayani Mbarali na Ileje mkoani Mbeya, viwanda viwili vya kusindika mazao ya bustani vimejengwa jijini Mbeya na Manispaa ya Mpanda/Katavi, masoko mawili ya kuuzia mazao ya bustani mawili katika wilaya ya Rungwe na Busokelo, na vikaushio vya mboga na matunda 15 vinavyotumia nishati ya jua (solar driers) kwenye baadhi ya Halmashauri zilizomo kwenye mradi wa KIBOWAVI.

# VITA YA SUKARI:



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe

# Mwanzo au mwisho wa mapambano?

**NA MWANDISHI WETU, FAMA**

Mkutano wa 15 wa Bunge la 12 ulifika ukomo wake Juni 28, 2024 ukiwa umegubikwa na suala la vita ya sukari ambayo kwa miaka na miaka imekuwa na tabia ya kung'oka na mawaziri wenye dhamana na bidhaa hiyo. Safari hii, vita vimebadili mwelekeo na kuishia kupigwa kofuli mbunge machachari, Luaga Mpina (Kisesa) ambaye amesimamishwa kuhudhuria vikao 15 vya Bunge.

Sukari ni miongoni mwa bidhaa nyeti, ikitumiwa kwa matumizi mbalimbali, ya nyumbani na viwandani. Sukari ni chakula, lakini ikiwa ni kati ya biadhaa zenye uhitaji mkubwa kwa matumizi ya kila siku ya binadamu.

Kulingana na taarifa za Bodi ya Sukari Tanzania (SBT), mahitaji ya sukari nchini ni wastani wa tani 650,000 kwa mwaka, hivyo kufanya biashara ya bidhaa hiyo kuwa ya thamani ya matrilioni ya shilingi. Kwa maana hiyo kuchangamkiwa na wengi kwa njia za halali na hata za hila. Ni kutokana na thamani ya biashara ya sukari kuwa kubwa ndiyo maana imebatizwa jina la 'dhahabu nyeupe'.

Ni katika kusaka mwarobaini wa kufikisha mwisho vita ya bidhaa hiyo ambayo imegharimu wengi nafasi zao nchini, wakiwamo mawaziri, kama ilivyokuwa kwa aliyekuwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Iddi Simba, Juni 27, 2024 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Sheria ya Fedha ya 2024 (Finance Bill 2024), ikiwamo ya mabadiliko ya sheria ya sukari. Muswada huo ndiyo ulihitimisha vikao vya Bajeti vilivyodumu kwa takriban miezi mitatu.

Katika sakata la sukari la mwaka 2001 Iddi Simba alilazimika kujiuzulu wakati wa utawala wa Rais Mkapa akituhumiwa kuwabeba wafanyabiashara kwa kuwapa vibali vya kuagiza sukari kinyume cha taratibu. Hili ndilo lilikuwa linafananishwa na la safari hii dhidi ya Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, likiwa limeshikiwa bango na Mpina, lakini ambacho mbunge huyo



**"LENGO LA HATUA HII NI KUWEZESHA UPATIKANAJI WA SUKARI NCHINI NA KUONDOA UHODHI KWA BAADHI YA WENYE VIWANDA BILA KUATHIRI DHAMIRA YA SERIKALI YA KULINDA VIWANDA VYA NDANI."**

**Mbunge wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina**

alisahau ni ukweli kwamba vibali vya sukari safari hii vilikuwa vimetolewa kwa Sheria ya Usalama wa Chakula kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA).

Pamoja na mambo mengine, kupitishwa kwa sheria ya fedha ya mwaka 2024 pia kulimaanisha mabadiliko ya sheria kadhaa zilizoguswa na Bajeti Kuu ya Serikali ambayo pia ilikuwa tayari imepitishwa na Bunge.

Sheria ya Sukari Na. 6 ya mwaka 2001, ni miongoni mwa Sheria zilizoguswa kwa kufanyiwa marekebisho yanayohusu uagizaji wa sukari kutoka nje ya nchi pale kunapotokea uhaba wa biadhaa hiyo kwa sababu zozote zile, hali inayoashiria kufikisha mwisho vita ya ukwasi wa bidhaa hiyo, 'dhahabu nyeupe'.

Mabadiliko hayo yanaweka kifungu kipya cha 14A katika sheria hiyo, kinachoruhusu NFRA kuagiza, kuhifadhi na kusambaza sukari kwa matumizi ya ndani ya nchi wakati wa upungufu wa bidhaa hiyo.

Akiwasilisha mapendekezo ya muswada huo bungeni Juni 21,2024, Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba, alizungumzia kuwekwa kwa kifungu hicho kipya cha 14A akisema:

"Lengo la hatua hii ni kuwezesha upatikanaji wa sukari nchini na kuondoa uhodhi kwa baadhi ya wenye viwanda bila kuathiri dhamira ya Serikali ya kulinda viwanda vya ndani." Awali Nchemba aliwasilisha kusudio la mabadiliko ya sheria hiyo ya sukari Juni 13, 2024 alipowasilisha bungeni Bajeti Kuu ya Serikali ya 2024/25.

Mabadiliko haya yanabadili utaratibu wa awali uliokuwa ukiwaruhusu wazalishaji wa sukari kwa kushauriana na Bodi ya Sukari nchini (SBT), kuagiza bidhaa hiyo kutoka nje pale kunapokuwa na upungufu.

Baadhi ya wachunguzi wa mambo wanasema mvutano uliokuwapo kuhusu sekta ya sukari ulitokana na mabadiliko ya sheria ambayo kimsingi yameondoa uwezekano wa makundi ya kimaslahi 'kutengeneza' uhaba wa sukari na kujinufaisha kwa upandishaji wa bei ambayo ni miongoni mwa bidhaa adhimu kwa ustawi wa jamii.

### Chimbuko la mabadiliko

Chimbuko la mabadiliko ya Sheria ni uhaba wa sukari nchini, uliosababisha bei ya bidhaa hiyo kupaa kutoka wastani wa Sh. 2,500 na 3,200 na kufikia kati ya Sh.4,500 na 10,000 katika baadhi ya mikoa nchini.

Takwimu za Wizara ya Kilimo zinaonyesha kuwa uzalishaji wa sukari katika msimu wa mwaka 2023/24 ulifikia tani 392,724, sawa asilimia 85.4 ya tani 460,048.94 zilizozalishwa msimu wa mwaka 2022/23. Pia uzalishaji huo ulikuwa chini ya kiwango cha tani 445,000 kilichokuwa kimesudiwa kuzalishwa.

Waziri ya Kilimo, Hussein Bashe, akiwasilisha makadirio ya matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka fedha 2024/25 bungeni, alizitaja mvua za El-Nino zilizonyesha kuanzia mwishoni mwaka 2023 hadi mwanzoni mwa 2024 kuwa sababu kuu ya kushuka kwa uzalishaji, kwani viwanda vilishindwa kuzalisha kutokana na miundombinu kwenye mashamba kuharibiwa na maji.

Bashe aliliambia Bunge kuwa uhaba wa sukari ulioendelea kuwapo baada ya kukoma kwa mvua za El-Nino ulitengenezwa kwa makusudi (artificial scarcity) na wafanyabiashara ambao hawakutumia vibali walivyopewa kuingiza sukari ili kuziba pengo (gap sugar), hivyo kujinufaisha na ongezeko la bei.

"Serikali ilikabiliwa na tatizo la upungufu wa sukari ambao ulitokana na mvua za EL-Nino na tabia za wafanyabiashara kutengeneza uhaba wa sukari (artificial scarcity) kwa kutokuingiza sukari ya kuziba pengo (gap sugar) kulingana na vibali vya uagizaji walivyopatiwa na hivyo kupandisha bei ya sukari," alisema Bashe na kuongeza:

"...ninaomba niwaambie wamiliki wa viwanda vya sukari nchini kuwa sukari ni chakula cha Watanzania masikini na ni suala la usalama wa

## Jedwali: Uchukuaji wa vibali msimu wa 2022/2023

| NA. | JINA LA KAMPUNI | TAR. YA KUCHUKUWA KIBALI |
|---|---|---|
| 1 | Kilombero | 30/03/2023 |
| 2 | Mtibwa | 14/04/2023 |
| 3 | Kagera Sugar | 14/04/2023 |
| 4 | TPC Limited | 03/05/2023 |
| 5 | Bagamoyo Sugar | Haikuchukuwa kabisa |

nchi, hivyo, Serikali haitavumilia wala haitaruhusu tena tatizo lililotokea kujirudia, ni wajibu wetu kuvilinda viwanda vya ndani, lakini ni wajibu wetu pia kuwalinda Watanzania na usalama wa nchi."

Kutokana na hali hiyo, Serikali iliwatumia NRFA kuratibu uingizaji wa tani za sukari 410,000, hatua ambayo Mbunge wa Kisesa, Luhaga Mpina aliikosoa akisema kiasi kilichotakiwa kilikua tani 120,000 tu, na kwamba uamuzi wa NFRA kuruhusu wafanyabiashara kuagiza sukari utaua viwanda nchini.

**Uhaba ulikoanzia**

Hata hivyo chagamoto ya uhaba wa sukari ulianza mwishoni mwa msimu wa 2022/23, pale wazalishaji walipochelewa kwenda Bodi ya Sukari Tanzania (SBT) kuchukua vibali vya kuingiza bidhaa hiyo kutoka nje ya nchi ili kufidia nakisi iliyokuwa imejitokeza mwishoni mwa msimu huo.

Mkurugenzi Mkuu wa SBT, Prof. Kenneth Bengesi, anasema uagizaji wa sukari pia huzihusisha taasisi nyingine ambazo ni Mamlaka ya Mapato (TRA), Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ambalo kimsingi ndiyo mamlaka ya udhibiti ubora, lengo likiwa ni kuhakikisha usalama wa bidhaa na bei.

Katika muktadha huo, Prof. Bengesi anasema SBT iliwaandikia wazalishaji kwenda kuchukua vibali vya kuingiza sukari tangu Machi 20, 2023 na kwamba kampuni ya kwanza ambayo ni Kilombero ilichukua kibali chake Machi 30, 2023.

"Kampuni mbili za Kagera na Mtibwa walichukua Aprili 14, 2023, Kampuni ya TPC ilichukua kibali chake Mei 3, 2023 na Kampuni ya Bagamoyo haikuchua kabisa kibali chake," anasema Bengesi na kuongeza kuwa kati ya vibali vilivyochukuliwa ni Kilombero pekee walioingiza sukari (tani 2,380) kwa msimu huo.

**Uhaba wa sukari**

Kutoingizwa kwa kiasi chote cha sukari kilichoidhinishwa na SBT kulisababisha kukosekana kwa sukari ya ziada kwenye mzunguko wa soko, hali iliyosababisha, bei kupanda ilipofika Juni 2023, hivyo kuchangia kuathirika kwa utengamano wa soko katika msimu wa uzalishaji wa 2023/2024.

Msimu huo mpya pia uliathiriwa na mvua za El-Nino ambazo kwa mujibu wa SBT, ulisababisha uzalishaji kusimama katika viwanda vyote isipokuwa Kilombero na Kagera, ambavyo havikuathirika sana, hivyo kuendelea na uzalishaji japokuwa chini ya uwezo wake.

Machi 2024, uongozi wa Kiwanda cha Sukari cha Mbigili kinachomilikiwa na Kampuni ya Mkulazi mkoani Morogoro, ulilimbia jarida la FAMA kwamba walilazimika kusitisha uzalishaji kwa muda kutokana na mvua za El-nino.

"Mvua kubwa zinaponyesha uvunaji unakuwa mgumu maana mashamba hayaingiliki, na hata tukifanikiwa kuvuna tunashindwa kusafirisha miwa kwenda kiwadani kwani magari ya ubebaji yanashindwa kuingia au yanakwama mashambani kutokana na miundombinu kuharibika," alisema Meneja Kilimo wa Kiwanda hicho, Flavian Reginald.

Kwa kuzingatia Sheria ya Sukari Sura ya 251 kifungu cha 14 (3)(b)(v) (ilivyokuwa wakati huo kabla ya marekebisho yaliyofanywa kupitia Sheria ya Fedha ya 2024), kushindwa kwa wazalishaji kuingiza sukari katika msimu wa 2022/2023 kuliwapotozea sifa ya kupewa tena vibali katika msimu uliofuata wa 2023/2024.

Hata hivyo, pamoja na kuwapo kwa takwa hilo la kisheria, taarifa zinaonyesha kuwa SBT ilitoa tena vibali kwa kampuni za wazalishaji, Kilombero walichukua kibali Januari 4, 2024 Kagera na Mtibwa na TPC walichukua Januari 5, 2024 na Bagamoyo wakachukua kibali Februari 2, 2024.

Profesa Bengesi anasema baada ya kuona mwenendo wa uingizaji wa kampuni za wazalishaji haueleweki, na ikizingatia kwamba msimu uliotangulia zaidi ya nusu ya waliopewa vibali hawakuingiza sukari na kusababisha uhaba, Serikali iliamua kuchukua hatua kuhaikisha sukari inaingizwa nchini kupitia NFRA.


Kwa upande wake Waziri wa Kilimo, Bashe anasema kwa kuwa katika mwaka wa fedha 2023/24 NRFA hawakuwa wametengewa fedha kwa ajili ya dharura ya sukari, walitumia sheria ya kuundwa kwao kuingia mikataba na baadhi ya kampuni binafsi ambazo ziliingiza kiasi kikubwa cha sukari kinachozidi kile kilichoingizwa na wazalishaji.

Profesa Bengesi alisema kila mzalishaji alipewa kibali cha kuagiza tani 10,000, lakini hakuna hata mmoja aliyeagiza kiwango hicho. Taarifa za SBT zinasema kuwa hadi kufika Februari 29, 2024 Kilombero walikuwa wameingiza nchi tani 3,100.5 kwa mikupua mitano; Kagera



**Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Sukari Tanzania (SBT), Prof. Kenneth Bengesi**

**"MVUA KUBWA ZINAPONYESHA UVUNAJI UNAKUWA MGUMU MAANA MASHAMBA HAYAINGILIKI, NA HATA TUKIFANIKIWA KUVUNA TUNASHINDWA KUSAFIRISHA MIWA KWENDA KIWADANI KWANI MAGARI YA UBEBAJI YANASHINDWA KUINGIA AU YANAKWAMA MASHAMBANI KUTOKANA NA MIUNDOMBINU KUHARIBIKA," ALISEMA MENEJA KILIMO WA KIWANDA HICHO, FLAVIAN REGINALD.**




Sugar tani 1,485; Mtibwa tani 1,485 wakati TPC walikuwa hawajaagiza chochote.

SBT ilisema kuwa kampuni ya Itel East Africa katika mikupuo mitatu, waliingiza jumla ya tani 25,750 peke yao. Wazalishaji wa sukari walitarajiwa kuingiza nchini walau tani 40,000, lakini walifanikiwa kuingiza jumla ya tani 6,070.5 tu kiwango ambacho hakikufikia hata kibali cha mwagizaji mmoja cha tani 10,000.

**Mvutano serikali, wazalishaji**

Baada ya NRFA kufanikisha uratibu wa kuwezesha kupatikana kwa suluhu ya uhaba wa sukari, Serikali ikafanya uamuzi wa kufanya marekebisho ya Sheria, uamuzi ambao ulisababisha mchakato wa marekebisho hayo kukumbwa na upinzani kutoka kwa wazalishaji wa sukari, wakisema mabadliko hayo yataathiri soko la ndani, huku wakikanusha tuhuma za 'kutengeneza' uhaba wa biadhaa hiyo na kusababisha bei yake kupanda.

Kamati ya Bunge ya Bajeti kupitia kwa Mwenyekiti wake, Oran Njenza, ilihadharisha kuwa kwa sasa NFRA haina uwezo wa kifedha wa kuagiza sukari kutoka nje ya nchi kwani ilikuwa imetengewa bajeti ya kununua nafaka na siyo sukari. Njeza alisema hali hiyo inaweza kusababisha NRFA kushindwa kutekeleza jukumu lake, kama yangetokea maafa.

Hata hivyo, Serikali ilisisitiza kuwa mabadiliko ya Sheria ni muhimu ili kuwezesha kuwapo kwa utulivu wa bei ya sukari na kuukabili upandaji wa mara kwa mara uliokuwa ukisababisha maumivu kwa walaji. Hatimaye Bunge lilipitisha muswada huo na baadaye kuwa sheria baada ya kusainiwa na Rais.

Wakati wa mchakato huo, Mbunge Mpina alijikuta akisimamishwa kuhudhuria vikao 15 vya Bunge kwa kosa la kumdharau Spika na kuonyesha dharau kwa Bunge. Alithibitika kutoa ushahidi hadharani kabla ya suala alilolifikisha kwa Spika halijahitimishwa.

Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilibainisha kuwa Mpina alikiuka itifaki ya bunge, kwani vielelezo vya ushahidi wa madai aliyoyatoa dhidi ya Waziri wa Kilimo (Bashe) kwamba alilidanganya Bunge kuhusu uagizaji wa sukari kutoka nje ya nchi, aliutoa katika vyomo vya habari kabla Bunge halijafanya uamuzi.

Kwa upande mwingine, viongozi wa Chama cha Wazalishaji Sukari Tanzania (TSPA) walitoka hadharani wakikana tuhuma za kushindwa kuagiza sukari kutoka nje ya nchi ili 'kupanga' uhaba na kuhodhi bidhaa hiyo ili kupandisha bei. Pia walisema Serikali iliwapa vibali kwa kuchelewa huku kampuni za kibiashara (zisizo na sifa) zikipewa kipaumbele cha kwanza cha vibali vya uagizaji wa bidhaa hiyo.

Mwenyekiti wa TSPA, Balozi Ami Mpungwe, alisema walikuwa wametoa hadhari mapema kwa serikali kuhusu uwezekano wa kutokea kwa upungufu wa uzalishaji kwa sababu za kuwapo kwa utabiri wa mvua za El Nino na kusisitiza kuwa vibali vya kuagiza bidhaa kutoka nje vilichelewa, hivyo kuathiri usambazaji.

Hata hivyo, baadaye uongozi wa SBT nao ulitoka hadharani na kuweka wazi jinsi mchakato wa utoaji wa vibali ulivyofanyika, ukionyesha kuwa licha ya wazalishaji wa sukari kupewa vibali vya uagizaji mapema, hawakufanya hivyo. Takwimu zinaonyesha kuwa kampuni za biashara ambazo baadaye zilipewa vibali na NFRA, ziliingiza kiasi kikubwa cha sukari, hivyo kuwezesha upatikanaji wa bidhaa hiyo kwa bei himilvu.

# Usichukulie mbegu ya miwa poa, inahitaji miaka 15 kumfikia mkulima



**NA FARAJA MASINDE, FAMA**

WATU wengi wanatumia sukari inayotokana na miwa, lakini ni wachache wanaofahamu mchakato wa kupata mbegu bora ya miwa ili bidhaa hiyo tamu iweze kufika mezani.

Undani huu wa mchakato wa mbegu bora za miwa unaelezwa kwa kina Bodi ya Sukari Tanzania (SBT), mamlaka yenye dhima ya kusimamia sekta ya sukari nchini, ikiwa ni pamoja kuiendeleza na kusaidia utafiti katika zao la miwa na kilimo chake kwa ujumla.

Kwa maana hiyo Bodi ya Wakurugenzi ya SBT ikiongozwa na Mwenyekiti wake inao wajibu wa kutoa miongozo ya kisera na maelekezo kwa Menejimenti kupitia Mkurugenzi Mkuu, ili kuhakikisha kuwa malengo yaliyowekwa yanafikiwa.

Mkurugenzi wa Mipango na Maendeleo wa Bodi ya Sukari Tanzania (SBT), Violeth Mwanisawa, anasema moja ya majukumu yao ni kuhakikisha wanaendeleza zao la miwa nchini, ambalo ni sehemu kubwa ya malighafi katika uzalishaji wa sukari.

Mwanisawa ambaye pia ni Mtaalamu wa Kilimo anasema wamekuwa wakishirikiana na Taasisi ya Kilimo Tanzania (TARI) kupitia Kituo chake cha Kibaha (TARI Kibaha) ili kuhakikisha wakulima wanapata mbegu safi na salama.

"Ikumbukwe kuwa SBT ni mwanachama katika kituo cha TARI Kibaha, hivyo tulishiriki katika majadiliano ya utafiti wa kupata mbegu ambazo zinafaa kwa wakulima.

"Tumepata mbegu aina mbili ambazo ni za hapa nchini za Taska I na Taska II, lakini mbegu nyingine ambazo ni nne, ni zile ambazo SBT ilikuwa na mradi kupitia andiko

ambalo lilituwezesha kupata fedha kutoka Common Fund for Commodities (CFC).

"Hawa walitusaidia kupata fedha za kununua mbegu tulizoziagiza kutoka nje na zikapelekwa kwenye karantini yetu pale Kibaha na baadaye zikaenda kujaribiwa kwenye mazingira ya wakulima, hivyo tumekuwa tukishirikiana kwa karibu katika kuandaa na kuhakikisha kuwa wakulima wetu wanapata mbegu bora na salama," anasema Mwanisawa.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa SBT, Profesa Keneth Bengesi anasema mbali na TARI kufanya utafiti wa mbegu bora nchini, SBT nayo imekuwa na mchango wake katika kuhakikisha kuwa kunakuwa na mbegu bora za miwa ili kupata sukari safi inayohitajika.

"Mara nyingi tunafanya hivi hasa kwenye mbegu zinazotoka nje ya nchi, kwani tunaagiza na zikifika nchini zinaingia katika karantini ya TARI wanazipokea na kuweka kwenye closer (karantini ya ndani), zinaweza kuwa aina 20 au 100... wanaangalia ambazo hazina magonjwa wanazipeleka kwenye karantini ya wazi kuangalia ufanisi wake kwenye mazingira hayo. Hatua hii huchukua mpaka miaka 15.

Profesa Bengesi anasema mbegu zinazothibitika kuwa sahihi na bora husambazwa kwa wakulima wakubwa nchini na hapo SBT inahuska.

"Sisi huwa tunanunua mbegu kisha tukakwenda kutengeza vitalu kwa wakulima wadogo, na kwa wale wakubwa tunawapa mbegu na mbolea bure, ikiwamo ardhi na kuwaambia kuwa mbegu zikiwa tayari waziuze labda kwa nusu bei ili wakulima wengi waweze kunufaika," anasema Prof. Bengesi na kuongeza:

"Tumekuwa na kitalu cha mbegu mkoani Manyara ambako mbegu tayari zimetolewa kwa wakulima na hili hufanyika kwa miaka miwili na baada ya hapo ile miwa ikianza kuvunwa manufaa yatakuwa ni ya yule mkulima ambaye amefanya kazi hiyo na sasa atauza mbegu kwa bei ya soko."

**Kwa nini miaka 15?**

Prof. Bengesi anasema utafiti kuchukua muda mrefu ni hatua za kisayansi na kwamba hata shambani zinakaa muda mrefu. "Miwa ni tofauti na mazao mengine kama mahindi, hivyo ndiyo sababu tunachukua muda mrefu kufanya utafiti," anasema Prof. Bengesi.

Kuhusu gharama za kuzalisha mbegu za miwa, Prof. Bengesi anabainisha kuwa unapoagiza kutoka nje inapofika hauwezi kuitumia bure, badala yake lazima uilipie kwa aliyeizalisha.

"Mfano, ukiagiza mbegu kutoka Afrika Kusini inapokuja hutaitumia bure, utatakiwa kuilipia kwa mzalishaji, hivyo kila unapokuwa unazalisha sukari utakuwa unailipia kwa miaka takribani 10 ndiyo inaweza kuwa bure, hivyo unaona kwamba hiyo tu yenyewe ni biashara kuliko unavyozalisha miwa ya kusaga kiwandani kwa ajili ya kuzalisha sukari.

"Gharama inakuja sababu uzao unaupata kwenye mbegu mwaka wa kwanza na wa pili unakuwa hauzai sana, lakini unatumia gharama kubwa kuhakikisha kuwa unapata mashina mazuri yaliyostawi vizuri na kutoa watoto ambao wana afya. Lakini uzao wake wastani unakuwa tani 50 kwa hekta, ila unapokwenda kwenye uzao wa tatu na kuendelea uzao wake unakuwa tani hadi 100,000, hivyo kadri miaka inavyozidi kusonga ndivyo kiwango cha uzalishaji kinaongezeka," anasema Prof. Bengesi.

Anafafanua kuwa mtazamo wa bodi sasa hivi ni kuchagua wakulima wa mfano ambao watapewa mafunzo kwa kushirikiana na TARI Kibaha ili wao wajikite katika kuzalisha mbegu tu badala ya kuzalisha miwa.

"Kwani kama tunavyofahamu kwamba ukikosea kwenye mbegu unaweza ukahamisha magonjwa mengi, hivyo tunataka tuwajengee uwezo ili watengeneze mbegu zinazohitajika sokoni," anasema Prof. Bengesi.

**SBT na TARI Kibaha**

Kwa upande wake Mwanisawa anasema SBT pia ina wataalamu ambao wamesomea kilimo hivyo wanajua hatua kwa hatu namna gani ya kupata mbegu bora.

"Kimsingi sisi pia tuna wataalamu ambao wamesomea kilimo, kwa mfano mimi pia nimesoma Agriculture Business and Agriculture Economics kwa hiyo najua hatua zote za namna gani tafiti za kupata mbegu safi na salama zinatakiwa zifanywe.



**Moja ya vitalu vya mbegu za miwa katika mashamba yanayosimamiwa na Bodi ya Sukari Tanzania (SBT).**

"Hivyo kuanzia mwanzo, Kibaha wanatekeleza, lakini katika utekelezaji ule SBT tunatoa utaaalmu wetu kupitia kamati ambayo pia ikihusisha wataalamu kutoka katika taasisi mbalimbali za sukari," anasema Mwanisawa.

Mtaalamu huyo anafafanua kuwa aina za mbegu zina tofautiana kwani zipo zile ambazo zinahitaji kumwagiliwa na nyingine ambazo ni kinyume chake.

"Mfano, kuna mbegu ambazo zinalimwa kwenye viwanda vya sukari zinahitaji uzimwagilie, sasa katika mazingira ambayo wakulima hawana miundombinu ya umwagiliaji, wengi wanatumia mbegu ambazo zinafaa katika mazingira ya mvua peke yake bila kumwagilia.

"Bila kumwagilia unalima unategemea mvua, lakini unapata mazao ingawa tija haitakuwa kubwa sana ikilinganishwa na anayemwagilia na kuna mbegu ambazo ukiziweka katika mazingira ya mvua pekee haziwezi kufanya vizuri kabisa.

"Kwa hiyo mbegu tulizozipata sisi ambazo zimetolewa na TARI ni hizo ambazo zinafaa katika mazingira ya mvua pekee na tija inakuwa kubwa. Kwa hiyo tunasema kwamba hizi zinafaa kwa wakulima kwa sababu hawana miundombinu ya umwagiliaji," anasema Mwanisawa.

**Gharama za mbegu**

Mtaalamu huyo anasema kuwa moja ya jukumu la bodi ni kuhakikisha kwamba hakuna mbegu ambayo itaingia kutoka nje ya nchi bila kuwa na kibali cha bodi.

"Bodi ndiyo inatoa kibali cha kuagiza mbegu hizi kutoka nje ya nchi, pia kuna taratibu nyingine ambazo zinatoka ndani ya Wizara ya Kilimo, pamoja na hayo na sisi bodi lazima tuidhinishe. Lakini unapozungumzia gharama, hizi mbegu zipo za aina mbili kama ilivyoelezwa kuwa kuna za mvua na za kumwagilia.

"Zile ambazo zinategemea mvua gharama yake unaweza ukaiona kama ndogo ikilinganishwa na hizi za umwagiliaji ambazo gharama zake ni kubwa sana, japo zinabebwa na kiwango cha uzalishaji wake kwani zinazaa mazao ya kutosha na mazuri.

"Lakini, upande wa bei mkulima anapokwenda kununua, bei hazitofautiani bila kujali hizi ni za kumwagilia au za mvua," anasema Mwanisawa.

Maendeleo sekta ya sukari

Mwanisawa anasema kuwa SBT ina majukumu ya kudhibiti na kuendeleza na kwamba katika hilo wanawaendeleza wakulima wa miwa kwa kuhakikisha kuwa wanapata mbegu safi na salama.

"Tunahakikisha wakulima wanapata vitalu vya mbegu zilizotolewa na TARI ili wote waweze kupata mbegu safi na salama. Mbegu za umwagiliaji tunaona kwamba ni vyema tukawawezesha wakulima wakapata miundombinu ya umwagiliaji ili waweze kuzalisha zao hili la miwa kwa kutumia zile mbegu ambazo zinafaa katika mazingira ya umwagiliaji ili tija ya kilimo hiki iongezeke.

"...tulianza katika mwaka wa fedha wa 2022/23 tuna mradi wa majaribio ulioko Kilombero ambapo tumebainisha vitalu shamba vya hekta 100 ambavyo tutajenga miundombinu ya umwagiliaji na kwa sasa tuko katika hatua za mwisho ili tuweze kuwasaidia wakulima hawa," anaeleza.

Mwanisawa anasema SBT pia inafanya kazi kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Umwagiliaji ambayo inasimamia matengenezo ya miundmbinu ya umwagiliaji katika maeneo ya kilimo.

Kuhusu miundombinu ya barabara isiyo mizuri kmashambani, Mwanisawa anasema wanatumia mfuko unaofahamika kama Sugar Industry Development Trust Fund (SIDTF) kusaidia ukarabati wa baadhi ya barabara za kusafirishia miwa mashambani.

"Mfuko huu kwa sasa unagharimia shughuli za utafiti na mafunzo ambayo yanatolewa na Chuo cha Sukari cha Taifa, lakini tunataka tuongeze wigo wa majukumu kwa kutumia fedha za mfuko kukarabati miundombinu ya barabara," anasema na kuongeza kuwa miundombinu mibovu ina athari kubwa kwa wakulima.

Mwanisawa anafafanua kuwa athari hizo ni uwezekano wa kuharibika kwa miwa kabla ya kufikishwa kiwandani. "Muwa ukichelewa kufika kiwandani zaidi ya saa 72 unakuwa haufai tena kwa ajili ya matumizi ya sukari," anasema Mwanisawa.



# NFRA:

# Mlima wa kufikia hifadhi tani milioni moja

**NA GRACE MWAKALINGA, FAMA**

ZIKO nyakati ambazo nchi yetu imewahi kutikiswa na uhaba wa chakula kutokana na majanga mbalimbali, iwe mafuriko au ukame au sababu nyingine zozote. Katika nyakati hizo waathirika kupitia viongozi wao huomba chakula cha msaada ili kuwawezesha kupata nafuu ya maisha.

Pengine swali kwa watu wengi ni je, chakula hiki cha msaada hutoka wapi? Jibu ni kwamba msaada wowote wa chakula ndani ya nchi, hutolewa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA - National Food Reserve Agency).

Hivyo jukumu kuu la NFRA ni kununua, kuhifadhi na kutoa chakula cha msaada katika maeneo yenye upungufu na waathirika wa majanga mengine, kama walivyofanya mwaka 2013 katika mikoa kadhaa nchini ambayo ilikumbwa na changamoto ya uhaba wa chakula.

Wakati huo aliyekuwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Christopher Chizza alinukuliwa akisema Serikali iliidhinisha kutolewa kwa tani 40,000 za mahindi kutoka ghala la chakula la taifa kwa ajili ya mikoa ambayo ilikuwa ikihitaji msaada.

Mikoa hiyo ilikuwa ni pamoja na Arusha, Dodoma, Kilimanjaro, Lindi, Mara, Manyara, Morogoro na Mwanza. Mingine ilikuwa Shinyanga, Singida, Tabora, Tanga, Mtwara, Pwani, Simiyu na Dar es Salaam ambako upungufu ulionekana kutokana na uhaba wa nafaka kwenye masoko pamoja na kupaa kwa bei.




Meneja wa NFRA Kanda ya Kati, Catherine Shangali

**NRFA HUTEKELEZA MAJUKUMU YAKE NCHI NZIMA KUPITIA KANDA NANE AMBAZO ZIMEUNDWA KIMKAKATI; KWANZA NI KANDA YENYE UZALISHAJI MKUBWA WA NAFAKA (MAKAMBAKO, SONGEA, SUMBAWANGA NA SONGWE), KANDA ZENYE UZALISHAJI WA WASTANI (DODOMA NA ARUSHA) NA UKANDA WENYE UZALISHAJI MDOGO (KIPAWA NA SHINYANGA).**

NRFA hutekeleza majukumu yake nchi nzima kupitia kanda nane ambazo zimeundwa kimkakati; Kwanza ni kanda yenye uzalishaji mkubwa wa nafaka (Makambako, Songea, Sumbawanga na Songwe), kanda zenye uzalishaji wa wastani (Dodoma na Arusha) na ukanda wenye uzalishaji mdogo (Kipawa na Shinyanga).

Afisa Mtendaji Mkuu wa NFRA. Dk. Andrew Komba aliliambia FAMA kuwa kwa sasa maghala waliyonayo yana uwezo wa kuhifadhi tani 361,000 za nafaka, huku wakiwa na kibarua cha kujenga uwezo wa kuhifadhi tani milioni moja ifikapo mwaka 2025/2026.

**Malengo la NFRA**

Julai 16, 2024 Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan alizindua vihenge na maghala ya kisasa ya NFRA, katika



Vitu vinavyotumiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kuwafundisha wakulima jinsi ya kuchambua nafaka kabla ya kuzipeleka kwenye ghala kwa ajili ya kuuza kwa ajili ya hifadhi. Picha na Eben Mitimingi.

eneo la Kanondo, mkoani Rukwa hatua ambayo imeongeza uwezo wa kuhifadhi nafaka kutoka tani 33,500 hadi 58,500. Ongezeko hilo la tani 25,000 linajumuisha vihenge vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 20,000 na maghala tani 5,000.

Awali Julai 14, Rais alizindua vihenge na maghala ya NFRA katika mkoa wa Mpanda mkoani Katavi yenye uwezo wa kuhifadhi tani 28,000 za nafaka.

Maghala yaliyozinduliwa Rukwa na Katavi yanatajwa kuwa na mfumo mzuri wa kupitisha hewa ambao pia unaoruhusu ufanisi katika uhudumiaji mazao (improved ventilation sytem and improved logistical system); ikiwa ni pamoja na utumiaji wa zana mbalimbali za kazi kama matrekta, mizani na vipandishi (elevators).

Uzinduzi uliofanywa Katavi na Rukwa ni mwendelezo wa kile Rais Samia alichokifanya Novemba 22, 2022 alipozindua vihenge na maghala ya kisasa yenye uwezo wa kuhifadhi tani 25,000 za nafaka katika Wilaya ya Babati, mkoani Manyara.

Afisa Mtendaji Mkuu wa NFRA. Dk. Andrew Komba anasema kukamilika kwa ujenzi wa miradi hiyo mitatu kunaifanya taasisi yake kuongeza uwezo uhifadhi kwa tani 78,000 zaidi na kufikisha uwezo wa kuhifadhi tani 361,000.

**Tani milioni moja**

Dk. Komba anasema hivi sasa NFRA katika malengo ya awali wanaendelea na ujenzi wa maghala mengine ili kuwawezesha kufikia tani 501,000.

Hata hivyo, Afisa Mtendaji Mkuu huyo anasema bado wana kibarua kikubwa zaidi kwani Serikali imewaongezea wajibu wa kuwa na maghala yenye uwezo wa kuhifadhi tani milioni moja katika mwaka wa fedha 2025/2026.

"Bado tunaendelea na ujenzi wa maghala maeneo mbalimbali nchini na tumeweka mikakati ya kufanikisha hilo kwa kukarabati maghala yaliyoko chini ya baadhi ya halmashauri ambayo yanaweza kutupa uwezo wa kuhifadhi tani 300,000 na kiasi kilichobaki ambacho ni tani 200,000 tutaihusisha sekta binafsi," anasema Dk. Komba.

NFRA ilianza kutekeleza mradi wa ujenzi wa maghala na vihenge Julai, 2019 baada ya kiasi cha Dola za Marekani milioni sita sawa na TSh. bilioni 14 kutengwa kwa ajili ya ujenzi, ili kusaidia uhifadhi za chakula nchini.

Dk. Komba anasema nafaka inayohifadhiwa kwenye maghala hayo huwekwa kwenye magunia yenye uzito wa kilo 50 hadi 90, kisha kupangwa kwa utaratibu maalum yakiwa juu ya chanja (pallets) zilizotandazwa juu ya sakafu na kufukizwa dawa ya kuua wadudu waharibifu.

"Wakati wote nafaka inapokuwa kwenye maghala huwa tunaifanyia ukaguzi wa ubora na kufukiza madawa pale inapohitajika," anasema Dk. Komba.

Uzalishaji wa chakula nchini

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe anasema katika msimu wa kilimo 2022/2023 uzalishaji wa chakula ulifikia tani milioni 20 ikilinganishwa na tani milioni 17 katika msimu wa kilimo wa 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 19.

Kadhalika mwaka 2022/2023, uzalishaji wa mazao ya nafaka ulikuwa tani milioni 11 ikilinganishwa na tani milioni tisa msimu wa kilimo 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 23.9. Uzalishaji wa mazao yasiyo nafaka ulikuwa tani milioni 8.9 ikilinganishwa na tani milioni 7.9 katika msimu wa kilimo 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 13.

"Uzalishaji wa mazao ya nafaka 2022/2023 ulikuwa tani milioni 11, mahitaji tani milioni 10 na ziada milioni moja, yasiyo nafaka tani milioni 8.9, mahitaji tani milioni 5.9 na ziada tani 2.9," anasema Bashe.

Kwa mujibu wa taarifa hizo za Wizara ya Kilimo, zao la mahindi linaongoza. Katika msimu wa 2022/2023 uzalishaji ulifikia tani milioni nane, ikilinganishwa na tani milioni sita zilizozalishwa 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 24.8. Bashe anasema mahitaji ya uzalishaji yalikuwa tani milioni 6.4, hivyo kuna ziada ya tani milioni moja.

Mpunga ni zao la nafaka la pili kwa uzalishaji ambalo mwaka 2022/2023 uzalishaji ulifika tani milioni mbili, ikilinganishwa na tani milioni moja zilizozalishwa katika msimu wa 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 36.5. Malengo yalikuwa ni kuzalisha tani milioni moja na ziada imebaki tani milioni moja.

# USALAMA WA CHAKULA:



Afisa Mtendaji Mkuu wa NFRA, Dk. Andrew Komba

## NFRA yaja na hatifungani



**Maghala ya kuhifadhia nafaka yaliyozinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan mkoani Katavi.**

**NA NEVILLE MEENA, FAMA**

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) unasubiri kwa shauku kuanza utekelezaji wa mpango wa hatifungani wa usalama wa chakula (food security bond), ili kuiwezesha taasisi hiyo kupata fedha za kujiimarisha kiteknolojia na kujenga uwezo wake wa kuhifadhi chakula nchini.

Kadhalika upatikanaji wa fedha hizo, utawezesha taasisi hiyo kupata vifaa bora kwa ajili ya kufanya tathimini ya mapema ya upatikanaji wa chakula ndani na nchi jirani pamoja na kuongeza ukubwa wa maghala ya kuhifadhia nafaka.

Afisa Mtendaji Mkuu wa NFRA, Dk. Andrew Komba, anasema ikiwa mpango huo utafanikiwa taasisi yake itajenga uwezo wa kutekeleza mpango wa mabadiliko makubwa ya kiteknolojia, ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa kufanya tathimini ya mapema ya uwezo wa uzalishaji (early warning system) wa ndani na nchi jirani.

"Mradi huu wa ku-apply (kutumia) 'early warning system' kujua uwezo wa uzalishaji wa nchi katika msimu husika utatusaidia sana kutuwezesha kujua hali itakuwaje kwa masoko, lakini pia kwenye uzalishaji wa ndani ya nchi na hata kwa nchi ambazo ni majirani zetu," anasema Dk. Komba na kuongeza:

"Kwa hiyo tuna mradi ambao tunauandaa wa food security bond yaani hatifungani za usalama wa chakula na tayari uko kwenye hatua za kupitishwa katika ngazi mbalimbali ndani ya serikali na utakapokamilika utatuwezesha kupata fedha za kutekeleza hii mipango yote ya kujiendesha kiteknolojia."

Julai mwaka huu Rais Samia Suluhu akiwa kwenye ziara mkoani Katavi alitangaza

azma ya Serikali kuanzisha hatifungani za usalama wa chakula ikiwa ni hatua ya kukusanya

fedha kwa ajili ya kuiwezesha NFRA kutekeleza majukumu yake na kulipa kwa wakati fedha za wakulima wanaoiuzia mamlaka hiyo nafaka.

Kadhalika Rais Samia alizungumzia suala hilo Agosti 8,2024 katika kilele cha maonyesho ya kilimo ya kitaifa ya Nane Nane jijini Dodoma akisema: "Tumezungumza na benki



**Maghala ya kuhifadhia nafaka yaliyozinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan mkoani Katavi.**



na wameunga mkono, hivyo tunakwenda kuweka hatifungani ya usalama wa chakula ambako tutapata fedha ambazo zitaiwezesha NFRA."

Msingi wa kuanzishwa kwa NFRA ni Sheria ya Wakala za Serikali Sura 245 (Na. 30/1997), kama ilivyorekebishwa na Sheria namba 13 ya mwaka 2009, ikisomwa pamoja na Hati Rasmi iliyoanzisha NFRA mwaka 2008 kupitia Tangazo la Serikali Na. 81 la tarehe 13 Juni, 2008 na kuhuishwa na Tangazo la Serikali Na. 120 la mwaka 2016.

Kwa mujibu wa Sheria hizo tajwa jukumu kuu la NRFA kununua, kuhifadhi na kutoa chakula cha msaada katika maeneo yenye upungufu na waathirika wa majanga mengine mbalimbali yanayoweza kujitokeza.

Akizindua ghala la kuhifadhia chakula lililogharimu Sh. bilioni 14, Rais Samia alisema mpango huo ni sehemu ya mkakati wa serikali kujenga uwezo wa kuhifadhi tani milioni 3 za nafaka ifikapo mwaka 2030, hatua ambayo anasema itaimarisha biashara ya nafaka baina ya Tanzania na nchi jirani.

"Mpango wa serikali ni kujenga uwezo wa kuhifadhi tani milioni 3 za nafaka ifikapo mwaka 2030 na tukitekeleza kaulimbiu ya kilimo biashara maana vijana wetu wanahitaji ajira, na hizo ajira sehemu kubwa tunazitarajia zitokane na kilimo," alisema Rais Samia.

**Mpango wa hatifungani**

Dk. Komba anasema utekelezaji wa uamuzi huo wa serikali kuhusu hatifungani za usalama wa chakula umeanza na kwamba wamekubaliana na Benki ya NBC Ltd kuwa mshahuri wa masuala ya kifedha (transaction advisor) ambaye atasimamia mchakato mzima wa uanzishaji wake akishirikiana na Serikali pamoja na taasisi nyingine.

"Katika hili NFRA tutauza hatifungani kwa wadau mbalimbali ambao watawekeza fedha zao, na sisi tutazitumia kufanya biashara ya nafaka na baadaye tutatumia fedha kutokana na hiyo biashara kuwarejeshea wahusika watakaokuwa wamewekeza fedha zao," anasema Dk. Komba.

Meneja wa Masoko na Mawasiliano wa Benki ya NBC, Godwin Semunyu, amethibitisha kuhusu benki hiyo kubeba jukumu la kusimamia mchakato mzima wa hatifungani za usalama wa chakula, ikishirikiana na Serikali kujenga muundo wa hatifungani zitakazowavutia wawekezaji kuzinunua na kutimiza lengo la Serikali kupata fedha za kuimarisha NFRA.

"Watu wanapojitokeza kununua hizo bond (hatifungani) lazima iwepo benki ambayo wajibu wake ndiyo inayotengeneza muundo mzima utakavyopaswa kuwa, kuonyesha fedha zitapatikanje na zitalipwaje, wawekezaji wajue watashirikije na mambo mengine; yote tutasimamia sisi Benki ya NBC," anasema Semunyu.

Taarifa za kitaalamu kuhusu masuala ya fedha zinataja majukumu ya taasisi yenye jukumu kama la NBC katika mchakato huu kuwa ni kuweka masharti ya hatifungani kama vile viwango vya riba, muda wake na hatua za kuchukua dhidi ya hatari zinazoweza kuhatarisha uwekezaji husika (risk mitigation measures).

**Tathmini ya hali ya chakula**

Kwa mujibu wa Dk. Komba miongoni mwa masuala yanayowekewa mkazo

katika mchakato wa kuimarisha taasisi hiyo, ni kujenga uwezo wa kufanya tathimini ya mapema ya upatikanaji wa chakula ndani na nchi jirani (early warning systems), ili kuwawezesha kujipanga kwa kuzingatia mahitaji halisi.

"Kwa mfano; mwaka huu NFRA tumejitahidi kununua mahindi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko katika nchi za Zambia na Malawi, lakini tumekuwa 'surprised' (tumeshangazwa) baada ya Zambia kusema kwamba wana njaa. Kama tungekuwa na mifumo inayoweza kukusanya taarifa za majirani zetu na hali waliyonayo kwa maana ya utoshelevu wa chakula, tungejipanga kuziba pengo hilo," anasema Dk. Komba na kuongeza:

"Kwa hiyo tunataka kwenda kwenye sayansi zaidi na utumiaji wa teknolojia katika kuendesha shughuli zetu, tofauti na zamani wakati NFRA alikuwa anasubiri mtu akija, tunanunua nafaka na tunaweka ghalani, kisha tunasubiri mteja. Sasa tutakuwa 'active' kwa maana ya kwamba tunatumia sayansi katika kuendesha operesheni zetu."

Afisa Mtendaji Mkuu huyo wa NFRA anasema mabadiliko mengine yanaendelea kufanywa kwenye ujenzi wa maghala ya kuhifadhia nafaka ambayo ni ya kisasa kwani yana uwezo wa kufanya kazi kadhaa bila kutegemea nguvu kazi ya watu wengi.

"Maghala tunayojenga sisi tunaita 'silos' ni ya kisasa kwani yana uwezo wa kufanya kazi nyingi tu; yanaweza kupima nafaka kama mahindi, kuisafisha nafaka hiyo, kuikausha kufikia kiwango cha unyevu tunachokihitaji, kupakia kwenye mifuko na kuingiza ghalani. Kazi zote hizo zinafanywa na mashine zenyewe tofauti na mifumo tuliyoizoea ambayo ni 'manual' (kuendeshwa na watu)."

**Ununuzi wa nafaka**

Kwa mujibu wa taarifa zilizoko kwenye tovuti ya taasisi hiyo (www.nfra.go.tz) nafaka zinazonunuliwa kwa sasa ni mahindi, mtama na mpunga na hununuliwa kupitia kanda mbalimbali za Wakala katika maeneo yaliyobainika kuwa na uzalishaji mkubwa nafaka.

Kwa maana hiyo, NFRA hununua chakula kutoka kwa wakulima kisha kukihifadhi kwa malengo yaliyotajwa. Hata hivyo, ziko nyakati ambazo kuliibuka malalamiko kutoka kwa baadhi ya wakulima kwamba wanapunjwa kiasi cha mazao wanapokwenda kuuza kwenye maghala ya wakala huyo ambaye ndiye mnunuaji mkubwa wa nafaka nchini.

Meneja wa NFRA Kanda ya Kati, Dodoma Catherine Shangali anasema kupitia utaratibu wa sasa wa ununuzi, NFRA wanatumia mizani ya kidijitali ambayo inamruhusu mkulima kuona kwa macho yake kiasi cha nafaka anachomuuzia wakala, lakini taarifa zote zinaingizwa kwenye mfumo ambao wakuu na wasimamizi wa taasisi hiyo wanaweza kuziona.

"Kupitia utaratibu wa sasa mkulima anaona uhalisia kiasi gani ambacho amepimiwa na pia anapatiwa risiti na wakati huohuo anapata ujumbe mfupi wa maandishi (sms) kwenye simu yake ya mkononi kupitia namba ambayo inakuwa imesajiliwa kwenye mfumo wetu wa ununizi wa mazao," anasema Shangali.

Kwa mujibu wa meneja huyo mkulima anapofikisha nafaka zake kwenye kituo cha kupokelea mazao anasajiliwa kwa taarifa zake zote kuingizwa kwenye kishikwambi, zikijumuisha majina yake, anuani yake kwa maana anakotokea, na aina mzigo wake.

"Pia huwa tunakagua hali ya mzigo, kwamba mzigo huo ukoje kisha tunatoa cheti cha ubora na tunatunza hizo taarifa kwenye mfumo wetu wa data. Baada ya hapo tunachukua nafaka husika na kupima kwa uzito wa kilo 50, tukizingatia uzito wa mfuko ambao huwa ni gramu 2. Kwa kuwa kila mzani wetu unaonyesha kila kitu kwa uwazi, mkulima anahakiki mwenyewe katika kila hatua," anasema Shangali na kuongeza:

"Taarifa zote hizo zilizoingizwa kwenye mfumo tunazipata tukiwa ofisini, mimi nikiwa kwenye ofisini nikifungua laptop yangu nikaingia kwenye mfumo wa ununuzi wa mazao katika kanda yangu ya Dodoma naweza kujua kila kituo kilichopo chini yangu kimenunua nafaka kiasi gani na kutoka kwa wakulima gani. Kwa hiyo nitasoma majina yao, aina ya nafaka iliyonunuliwa na kiasi kwa maana ya kilo au tani."

Shangali anasema mfumo huo umeondoa malalamiko mengi kutoka kwa wakulima pamoja na kuwezesha malipo kufanyika kwa haraka kwani taarifa zote muhimu zinakuwa zimetunzwa kwenye mfumo, huku zikiwa zimehakikiwa na mkulima anayekuwa amewauzia nafaka.

"Teknolojia hii imeturahisishia kazi kwani kipindi cha nyuma ilikuwa ni mpaka mtu apimiwe, watu waandike kwenye nyaraka kwa kutumia mkono na zitumwe makao makuu ya kanda ili ziweze kufanyiwa utaratibu wa malipo, lakini kwa sasa ni rahisi kwani nyaraka za malipo zinapatikana kwenye mfumo wa mauzo," anasema.



**Baadhi ya wananchi wakishiriki hafla ya uzinduzi wa vihenge vya kisasa vya kuhifadhia nafaka uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan (hayupo pichani) mkoani Katavi.**

# VETA ilivyowekeza kuinua kilimo

**MIONGONI mwa taasisi za umma ambazo huwezi kuzikosa kwenye maonyesho ya Kitaifa ya Kilimo (Nanenane) ni Mamlaka ya Vyuo vya Ufundistadi (VETA). Swali ambalo watu wengi pengine wanaweza kuwa nalo ni uhusiano wa taasisi hii iliyoko chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na masuala ya kilimo.**

**NA MWANDISHI WA FAMA, DODOMA**

Sitta Peter ambaye ni Meneja Uhusiano wa VETA ana majawabu ya swali hili na mengine kadhaa. Sitta anakiri kwamba wajibu wa VETA ni kutoa mafunzo ya ufundi stadi, ila mafunzo hayo kwa sehemu yanaigusa sekta ya kilimo.

Akizungumzia uwezo wa VETA, Sitta anasema: "...tunakuwepo kwenye maonyesho kama nanenane kwa sababu mambo makubwa mawili yanayohusiana na kilimo; la kwanza ni kuhusiana na hayo mafunzo ya ufundi stadi, kwamba tuna mafunzo ambayo yanalenga sekta ya kilimo."




**Wanafunzi wa fani ya uchinjaji na uchakataji wa nyama wa VETA Dodoma wakionyesha kwa vitendo kile wanachokisomea chuoni, wakati wa maonyesho ya Kilimo (nanenane) kitaifa, jijini Dodoma.**

Kwa mujibu wa Meneja Uhusiano huyo wa VETA, taasisi hiyo ina vyuo vitano vinavyotoa mafunzo ya ufundi stadi kwenye ufundi wa zana za kilimo. Vyuo hivyo ni Mpanda katika Mkoa wa Katavi, Dakawa na Kihonda mkoani Morogoro, Manyara na Oljoro mkoani Arusha.

"Vyuo hivi vinatoa mafunzo ya zana za kilimo, lakini tuna chuo chetu cha Veta Singida kinatoa mafunzo ya ufugaji wa mifugo ya aina mbalimbalio kwa hiyo nalo ni eneo linalogusa kilimo. Kwa sababu kilimo ni pamoja na ufugaji na huwezi ukavitenganisha," anasema Sitta na kuongeza:

"Pia kuna eneo la ufugaji wa nyuki ambao linajitegemea na hapa tuna chuo chetu cha Dakawa ambacho kinatoa mafunzo ya ufugaji wa nyuki."

Sitta anasema katika muktadha wa VETA kutoa mafunzo ya ufundi stadi kwenye maeneo mbalimbali yanayogusa kilimo, uwepo wao kwenye shughuli zozote za kitaifa zinazohusu sekta ya kilimo ni muhimu kwani wanapata fursa ya kuwaelimisha wananchi.

"Tunataka wakulima wafahamu kwamba wakitaka kuboresha kilimo na kulima kwa tija basi wanatakiwa wapate mafunzo, na sisi mafunzo tunayatoa VETA maana mafunzo ya ufundi stadi yanamfanya mtu aweze kutenda kazi moja kwa moja," anasisitiza Sitta.

### Mahitaji ya soko la ajira

Sitta anasema utoaji wa mafunzo ndani ya VETA unazingatia mahitaji ya soko la ajira na kilimo ni eneo mojawapo. Anaeleza kwamba hata mgawanyo wa vyuo vitano vinavyojihusisha na kilimo, vimepangwa kimkakati vikilenga kuzalisha wanafunzi na teknolojia zinazohitajika katika eneo husika.

"Kwa mfano ukienda Arusha na Manyara ndiko maeneo ambako kuna matumizi makubwa ya zana za kilimo kutokana na uwepo wa mashamba makubwa. Kwa hiyo sasa hata mahitaji ya vijana wenye utaalamu wa ufundi wa zana za kilimo ni makubwa.

"Ndiyo maana unakuta chuo cha VETA Manyara kinatoa mafunzo ya ufundi wa kilimo na chuo cha VETA Oljoro Arusha kinatoa mafunzo hayo ya zana za kilimo," anasema na kuongeza kuwa hata Mpanda nako ni eneo ambalo liko kwenye ukanda wa uzalishaji mkubwa, hivyo matumizi ya teknolojia ni makubwa.

Sitta anasema vyuo vya Morogoro na Dakawa vinalenga kuzalisha wataalamu ambao wanaweza kutatua changamoto za wakulima hasa wanaotumia matreka, katika maeneo ya Kilombero na Ifakara ambako kuna uhitaji mkubwa wa mafundi wa zana za kilimo.

"Lakini ukienda ukanda wa kati ni kwa wafugaji zaidi Singida, Dodoma na Tabora, maeneo hayo yana ufugaji mkubwa. Ndiyo maana chuo cha VETA kikachukua hilo jukumu la mafunzo ya ufugaji kwa




"WAKATI MWINGINE WAFUGAJI WANAZALISHA MAZIWA MENGI NA HAWANA SOKO NA WENGI WAKATI MWINGINE HUISHIA KUMWAGA.

**Mwalimu wa Chuo cha VETA, Dar es Salaam, Ally Idd Issa akitoa maelezo kwa watu waliotembelea banda la taasisi hiyo kwenye maonyesho ya kilimo (nanenane) kitaifa, jijini Dodoma.**

hiyo tunafanya kwa mtizamo huo," anasema Sitta.

Anasema kwa chou cha VETA Dakawa wanazingiatia ufugaji wa nyuki kutokana na kuwepo kwa misitu katika eneo hilo, hivyo kuona uwapo wa fursa ya kuanzisha na kutoa mafunzo katika eneo hilo.

"Nikisema ni upi mpango wa VETA, ni kwamba tuna mawazo ya kuongeza wigo hasa kupitia vyuo vya wilaya kwa sababu viko maeneo ya vijijni ambako shughuli kubwa za huko ni kilimo na ufugaji, tunawaza kwamba tuingize fani zinazohusiana sekta hizo mbili ili kusaidia wananchi kupata ujuzi na kufanya kilimo chenye tija,"anasisitiza Sitta.

Kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, serikali imekamilisha ujenzi wa vyuo 29 vya mafunzo ya ufundi na ufundi stadi na kati ya hivyo 25 ni vya wilaya na vinne ni vya kiwango cha mkoa. Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda anasema vyuo 25 vya VETA vya Wilaya vimeanza kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi.

"Serikali pia imeanza ujenzi wa vyuo 64 vya VETA vya wilaya kikiwemo Chuo cha VETA Chamwino ambapo ujenzi wa chuo hicho umefikia asilimia 83. Kadhalika Serikali imejenga chuo cha VETA cha kiwango cha Mkoa wa Songwe," alisema Mkenda wakati akiwasilisha hotuba ya makadirio ya wizara hiyo katika Bunge la bajeti.

**Ubunifu kusaidia kilimo**

Sitta anasema eneo la pili katika shughuli za mafunzo ya ufundi stadi ni ubunifu. "Walimu wetu wanabuni mashine na teknolojia za aina mbalimbali. Teknolijia hizo zinasaidia kwenye eneo la kilimo," anasema.

Anataja maeneo ambako ubunifu huo unafanya kazi kuwa ni vifaa vya umwagiliaji hasa wa bustani, mashine za kuchanganya vyakula vya mifugo na wana ubunifu wa mashine inayobadilisha maziwa ya maji kuwa maziwa ya unga ili kuyawezesha kuhifadhika kwa muda mrefu.

"Wakati mwingine wafugaji wanazalisha maziwa mengi na hawana soko na wengi wakati mwingine huishia kumwaga. Wakiwa na mashine ya aina hii, wanaweza kuyabadilisha kuwa ya unga, yakahifadhika yakakaa muda mrefu kipindi ambacho kuna uhitaji, yatatumika," anasema Sitta.

Anautaja ubinifu mwingine ndani ya taasisi hiyo kuwa ni ule uliofanywa na walimu wa VETA Dar es Salam ambao wamebuni mbolea na dawa za kuua wadudu shambani kwa kutumia teknolojia ya maabara.

"Kwa sababu VETA Dar es Salaam tunafundisha mafunzo ya maabara kwa kutumia teknolojia




**Afisa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mafunzo wa VETA, Joseph Kimako akionyesha udongo maalum unaotengenzwa na taasisi hiyo, kwa ajili ya kuandaa vitalu vya mazao ya bustani, kwenye maonesho ya kilimo (Nanenane) kitaifa, jijini Dodoma.**



**Mmoja wa wafanyakazi wa VETA (aliyevaa fulana ya bluu) akitoa maelezo kwa wananchi waliotembelea banda la taasisi hiyo kwenye maonyesho ya Kilimo (nanenane) kitaifa mkoani Dodoma.**

hiyo wanafanya ubunifu wa dawa mbalimbali na miongoni mwa dawa walizobuni ni zile za kuuwa wadudu waharibifu mashambani, lakini pia mbolea ambayo haina kemikali zile za viwandani," anafafanua Sitta.

**Ushirikiano na MATI na LITI**

Sitta anasema VETA imekuwa ikishirikiano na Vyuo vya Kilimo (MATI) na vile vya Mifugo (LITI) japokuwa, siyo imara. "Tulikuwa na mjadala hata na LITI kuona tunawezaje kuendesha mafunzo kwa pamoja, lakini kwa sasa tunachokifanya zaidi ni ushirikiano kwenye mafunzo ya muda mfupi na hasa yale ya kuwafikia wahitaji katika maeneo yao," anasema.

Sitta anatoa mfano wa mradi unaoitwa 'Tajirika na Kilimo' ambao uliendeshwa katika mikoa ya Njombe, Iringa na Morogoro kwa kushirikiana na vyuo vya mifugo kutoa mafunzo kwa wakulima na wafugaji katika maeneo hayo kwa njia ya kuwafikia waliko (outreach). Hata hivyo, anakiri kuwa "hatujawa na mkakati wa pamoja unaolenga kuendesha shughuli kwa ukaribu zaidi."

Hata hivyo anasema VEATA inaona muhimu wa kuimarisha ushirikiano na taasisi hizo mbili kwa kuzingatia kwamba zina uzoefu wa muda mrefu katika utoaji wa mafunzo yanayohusiana na kilimo na ufugaji, uzoefu ambao unaweza kuisadia mkakati wa VETA katika kuingiza mafunzo yake kwenye vyuo vipya vya wilaya vinavyoendelea kujengwa.

"Jambo la pili, kama nilivyosema VETA tunatoa mafunzo ya ufundi wa zana za kilimo, mafunzo ya ufugaji na ufugaji wa nyuki, hivyo tuna wataalamu wachache. Kutokana changamoto hiyo ya wataalamu katika maeneo hayo, walimu kutoka LITI na MATI wanaweza kutusaidia au tunaweza kutumia wataalamu wao kusaidia utoaji wa mafunzo kwenye maeneo ambayo tunalenga kuyaongeza," anasema Sitta na kuongeza:

"Ikumbukwe pia kwamba hizi taasisi zinafundisha hata vijana wenye kiwango cha elimu kama Diploma ambao tunaweza hata tukawaajiri, achilia mbali wataalamu walioko kwenye taasisi kama walimu. Wahitimu wake tunaweza kuwatumia kufundisha sasa kwenye vyuo vyetu."